

MTOTO AKIKUA

1. Samaki kumpatia, simngoje akauke,
Mbichi kimngojea, atakuja anyauke,
Itakuwa mazoea, iwe ndio kazi yake,
Mtoto akikua, tabiaye haiachi.
2. Gertrude nisikia, wewe sikasirike,
Kazi kuparamia, bora awe pweke,
Huyo haramia, hataweza mikeke,
Mtoto akikua, tabiaye haiachi.
3. Mkunje kimvua, wala sipumzike,
Inyooshe tabia, singojee ipindike,
Akisha kaukia, utaacha avunjike,
Mtoto akikua, tabiaye haichi.
4. Mtafutie njia, adabu aishike,
Aso kusikia, ufito mtandike,
Uki muachia, basi aharibike,
Mtoto akikua, tabiaye haichi.

*Yusuf M. Kalala
Washington D.C.*